

**HERI YA  
SIKU YA KUZALIWA**



## SOMA HADITHI HII

**Ilikuwa wakati wa sherehe ya siku ya kuzaliwa kwa Mikaeli. Alikuwa akisherehekea mwaka wa kumi wa kuzaliwa kwake.**

Marafiki wengi walikuja kwenye sherehe yake ya kuzaliwa. Kila rafiki alileta zawadi. Walicheza michezo, wakala keki na aisi krimu, na ukafika wakati wa Mikaeli kufungua zawadi zake nyingi.

Moja baada ya nyingine, Mikaeli alichukua kila zawadi na kuifungua — gari dogo la kimtindo, mpira wa futboli, nguo na saa nzuri sana ya mkononi. Hizi zawadi zote alipewa Mikaeli bure. Alipewa Mikaeli na marafiki waliompenda sana.

Mikaeli alifurahi sana. Akisherehekea kumbukizi ya kuzaliwa kwake miaka kumi iliyopita akiwa mtoto mchanga.

Zawadi ya mwisho aliyoifungua ilikuwa kutoka kwa rafiki yake wa karibu sana, Charles. Ndani ya zawadi kulikuwa na kipeperushi chenye swali. Hili ndilo swali lenyewe:

### **“JE, UMEJIUNGA NA FAMILIA YA MUNGU?”**

Swali hili lilimshangaza Mikaeli. “Je, nimejiunga na familia ya Mungu?” alijiuliza.

“Ala, Charles, unamaanisha nini, ‘Je, umejiunga na familia ya Mungu?’”

“Basi vizuri, je, wewe ni Mkristo?” aliuliza Charles.

“Huwa ninaenda kanisani, ndicho unachomaanisha,” alisema Mikaeli.

“Mikaeli lazima uzaliwe katika familia ya Mungu na kisha, unaweza kusherehekea sherehe mbili za kuzaliwa,” alisema Charles.

“Unanitania - sherehe mbili za kuzaliwa?” aliuliza Mikaeli.

Mikaeli alishangazwa zaidi kuliko wakati wote. Angewezaje kuwa mtoto mchanga tena? Angewezaje kujiunga na familia ya Mungu? Angewezaje kuwa Mkristo?

Je! Wewe ni kama Mikaeli? Je! Unashangaa pia? Unajua? Ikiwa haujui, endelea kusoma na utajua jinsi wewe pia unaweza kuwa na sherehe mbili za kuzaliwa:

1. Je! Unajua kuwa kila mtu amekosea? Biblia inasema: “Wote wamefanya dhambi (wamefanya vibaya).”
2. Je! Unajua Yesu alikufa msalabani kuchukua adhabu yako kwa mambo mabaya uliyoyafanya?

3. Je! Unajua kuwa Mungu alimtuma Mwanawe, Yesu, kama zawadi kwa ulimwengu wote?
4. Je! Unajua Yesu yu hai?
5. Je! Unajua kuwa Mungu anataka uwe Mkristo? Hii inamaanisha kuwa uzaliwe mara ya pili katika familia ya Mungu na sasa uwe na sherehe mbili za kuzaliwa! (Yesu alisema, "Lazima uzaliwe mara ya pili." Yohana 3:7).

## **SASA, je! ungependa maombi kuongea na Mungu katika sala kuhusu kujiunga na familia yake?**

1. Mwombe Mungu akusamehe kwa makosa yako. "Kwa maana wote wamefanya dhambi..." Warumi 3:23
2. Mwambie Mungu kwamba unaamini kwamba alimtoa Yesu kufa msalabani kwa ajili yako. "Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kulingana na maandiko." 1 Wakorintho 15:3
3. Mwambie Mungu kwamba unataka Yesu awe Mwokozi wako na Rafiki yako mwenyewe. "Kwa wote wanaompokea Yesu, aliwapa haki ya kuwa watoto wa Mungu." Yohana 1:12
4. Mshukuru Mungu, Baba yako wa Mbinguni, kwa kumtoa Yesu, Mwanaye. 2 Wakorintho 9:15
5. Mwambie mtu mwingine kwamba sasa wewe ni wa familia ya Kikristo ya Mungu. Luka 2:17

## **Tamka sala hii...**

*Mpendwa Baba wa Mbinguni:*

*Nisamehe kwa makosa ambayo nimefanya. Ninaamini Mwanao, Yesu, alikufa kwa ajili yangu kuchukua dhambi yangu.*

*Nisaidie kunena na kutenda kama Mkristo anavyopaswa kufanya.*

*Nisaidie kukufurahisha katika kila ninachofanya na kusema. Na sasa, nataka kukushukuru kwa Yesu, Mwanako, ambaye ananipenda na yuko tayari kunisaidia.*

*Amina*

## ***Naweza kutambua mimi ni Mkristo kwa sababu:***

### **...Biblia inaniambia hivyo.**

Wagalatia 3:26 inaniambia...mimi ni mtoto wake.

1 Yohana 1:9 inaniambia...Mungu ananisamehe.

Yohana 3:16 inaniambia...Mungu ananipenda.

Yohana 14:2-3 inaniambia...Nitaenda mbinguni.

Jina langu ni: \_\_\_\_\_

Nimekuwa mshiriki wa familia ya Mungu mnamo \_\_\_\_\_,

ambayo ni siku yangu ya kuzaliwa mara ya pili.

## ***Sasa kwa kuwa wewe ni Mkristo, na mshiriki wa familia ya Mungu...***

...Soma Biblia yako kila siku.

...Ongea na Mungu, Baba yako wa Mbinguni.

...Nenda kanisani kila juma.

...Waambie marafiki na jamaa habari za Yesu.

...Onyesha upendo na fadhili kwa kila mtu.

...Ujitoe kwa kila njia kuwahudumia Mungu.

*Hadithi hii imetolewa na:*



**FMP**  
Foursquare Missions Press

Imechapishwa na Foursquare Missions Press © 2003

Pamoja na Mizizi Mobile Missions Press © 2020

Imetafsiriwa kwa Kiswahili na Stacy Collins.

Imehaririwa na Peter Dalmas.

Happy Birthday-Swahili